HISTORIA YA WACHAGA

Ili kuitalii vyema historia ya wachaga hapa chini kuna ramani ya eneo la mji wa Moshi, mji wenye historia ndefu ya kweli na iliyochanganyikana na utani ndani yake. Kutokana na tabia ya wachaga kupenda sana pesa, baadhi ya watu hutania kuwa kirefu cha neno MOSHI ni Mungu Onesha Sehemu Hela Ilipo. Hebu sasa twende pamoja hapa chini tuwatalii hao wanaoitwa wachaga.

Ramani ya mji wa Moshi Chanzo >>>

**Usuli**

Wachaga ni kabila la watu wenye asili ya Kibantu lakini pia mchanganyiko wa damu, hasa ya Kikushi wanaoishi kaskazini mwa Tanzania chini ya mlima Kilimanjaro, mkoani Kilimanjaro.Shughuli kubwa ya Wachaga ni biashara, kilimo na kazi za ofisini.Wachaga ni kabila la tatu kwa ukubwa nchini Tanzania. Takwimu za mwaka 2003 zinaonyesha kuwa idadi ya Wachaga ni watu 2,000,000.

**Historia ya Wachaga**

Kabila la Wachaga linapatikana mkoani Kilimanjaro. Kwa asili, Wachaga ni mchanganyiko wa Wamasai, Wasambaa, Wataita, Wakamba na Wakahe. Wachaga walianza kuhamia kwenye miteremko ya Mlima Kilimanjaro kwenye karne ya 17.

Wachaga ni kabila la watu wenye asili ya Kibantu lakini pia mchanganyiko wa damu, hasa ya Kikushi wanaoishi kaskazini mwa Tanzania chini ya mlima Kilimanjaro, mkoani Kilimanjaro.Shughuli kubwa ya Wachagga ni biashara na kilimo.Wachagga ni kabila la tatu kwa ukubwa nchini Tanzania. Takwimu za mwaka 2003 zinaonyesha kuwa idadi ya Wachagga 2,000,000.

Wachaga wana historia ndefu ya asili yao na ya maingiliano yao na makabila mengine. Kabila la Kichaga ni mkusanyiko wa makabila madogomadogo (ya Kichaga) yaliyosambaa kijiografia

kuzunguka mlima Kilimanjaro kuanzia mashariki (Tarakea, Rombo) hadi magharibi kwa Kilimanjaro (Siha, Machame).

Makabila ya Kichaga ni Wa-Rombo, Wa-Vunjo ambao wanajumuisha watu wa Mwika, Mamba, Marangu, Kilema na Kirua ambayo ndio inajulikana na wengi kama Kirua Vunjo. Ukipenda unaweza kuwagawa watu hawa wa Vunjo kama Wa-Mwika, Wa-Mamba ,Wa-Marangu,Wa-Kilema,na Wakirua.Makabila mengine ni Wa-Old Moshi, Wa-Kibosho, na Wa-Machame, Wa-Uru, na Wa-Siha.

**Lugha ya Kichaga**

Lugha ya Kichaga inabadilika kuanzia unapotoka Tarakea mpaka unapofika Siha magharibi mlima Kilimanjaro.

Kutokana na tofauti hizo Kichaga kimegawanyika katika Kirombo (ambacho nacho kinatofautiana kadiri unavyotoka eneo moja hadi jingine; mfano Kisseri, Kimashati, Kimkuu, Kimengwe, Kimahida), Kivunjo, Kimarangu, Kirombo, Kioldimoshi, Kingassa, Kiuru, Kikibosho, Kimachame na Kisiha.

Lugha hizo zinakaribia kufanana kadiri makabila hayo yalivyopakana. Kwa mfano, Kivunjo kinafanana na Kioldimoshi. Vile vile Kisiha kinafanana sana na Kimachame ambacho pia kinafanana kidogo na Kikibosho.

Baadhi ya Wamachame walihamia sehemu za Meru, Arusha, na kuchanganyikana na Waarusha, hivyo lugha yao ikabadilika kidogo na kuwa Kimeru. Kwa sababu hiyo Wameru wanasikilizana sana na Wamachame ingawa lafudhi zao zinatofautiana kidogo.

**Koo za Kichaga**

Majina ya kiukoo ya Kichaga pia huashiria wanatoka sehemu gani ya Uchaga, japo si lazima kuwa hivyo: kwa mfano, familia maarufu za Kichaga nchini Tanzania ni kama ukoo wa akina Mushi, Mmasy Kimaro, Swai, Massawe, Lema, Urassa, Nkya, Ndosi, Meena hutoka Machame.

Akina Temu, Mlaki, Mlay, Lyimo, Moshiro, Mselle, Kamnde, Kileo, Kimambo, Tesha, Msaki, Assey, Kyara, Kessy, Ndanu, Macha, Mbishi, Kombe, Njau wanatoka Old Moshi na Vunjo.

Majina mengine ya Old Moshi ni kama yafuatayo: Mmari, Macha, Mshiu, Kyara, Moshi, Massamu, Kimambo, Mboro, Mlngu, Saule,Tenga, Njau, Malisa, Maro, Maeda, Ringo,Olomi, Ngowi, Lyatuu na mengine mengi.

Kavishe, Mariki, Tarimo, Laswai, Mallya, Mrema, Mkenda, Massawe, Silayo, Lyaruu, Makyao, Mowo, Lamtey, Tairo, Masue, Maleto, Mramba, Kauki wanatoka Rombo.

Sawe, Usiri, Shayo, Kiwelu, Makundi, Urasa, Mtui, Moshi, Meela, Minja, Njau,Mtei wanatoka Marangu na Kilema.

Rite, Makule, Minja, Mashayo, Chao, Shao, Makawia, Ndesano, Kimario, Tilla, Mariale, Tarimo, Mafole, Kituo, Mrosso, Lyakundia, Kessy, Mmbando, Matemba, Ndenshau, Morio, Akaro, Matowo, Towo, Mkony, Temba, Foya, Munishi, Kilawe, na kadhalika hutoka Kibosho.

Ukoo wa akina Teri wako Mamba, Chami, Chuwa, Kiria Owoya na wachache Sango, Old Moshi na wengine walihamia Maji ya Chai, Mkoa wa Arusha.

**Utawala wa jadi wa Wachaga**

Watawala wa Kichaga waliitwa "Mangi". Hawa walihodhi mashamba, ng'ombe na waliheshimiwa kama viongozi wa kikabila. Walikuwa na nguvu za kisiasa na utajiri. Baadhi ya Ma-mangi mashuhuri katika historia ni kama Mangi Rindi aliyeingia mikataba na wakoloni (Wajerumani), Mangi Sina wa Kibosho na Mangi Horombo wa Keni - waliojulikana kwa uhodari wao wa vita katika kupigana na Wamachame na kupora ng'ombe na mazao yao, hata

mpaka leo makabila ya Kimachame na Kikibosho hayaoani kwa urahisi, na Mangi Marealle wa Marangu na Vunjo. Mangi Meli huyu alikuwa mangi wa waoldmoshi ambaye alipigana na wajerumani na aliishia kukatwa kichwa na mpaka sasa kichwa chake kipo ujerumani alizikwa kiwiliwili tuu baada ya kumnyoga na mti aliyonyongewa upo mpaka sasa sehemu ya oldmoshi bomani karibu na kolila sekondari .

Wakoloni walipokuja Kilimanjaro waliingia mikataba na viongozi hawa wa kikabila ili kuweza kuweka misingi yao ya kikoloni. Pia ndugu na watoto wa Ma-mangi walikuwa wa kwanza kupata elimu ya kikoloni, kwa hiyo waliweza kushirikishwa katika serikali za kwanza. Hawa pia wanaaminika walikuwa kama mabepari wa kwanza wa kijadi, maana walifanyiwa kazi na watu wengine wakati wao Ma-mangi wamekaa kuhesabu mali zao.

Usemi maarufu wa "u-Mangi-meza" nadharia inawezekana kuwa umetokana na watawala hawa wa Kichaga.

**Elimu kati ya Wachaga**

Wachaga wanajulikana kwa uwezo wao mkubwa katika uwanja wa elimu, hususani katika masomo ya sayansi na hisabati. Moshi ni maeneo ya mwanzo ambayo wamisionari wa Ukristo walijenga makanisa na shule.

Sababu hii imefanya Wachaga kuwa kabila namba moja lenye watu wengi zaidi walio na elimu ya kisasa (elimu ya juu) na mkoa wa Kilimanjaro unaongoza kwa idadi ya shule za sekondari nchini Tanzania. Kulingana na takwimu za elimu mkoa huo una shule za sekondari zaidi ya 320. Pia mkoa una shule za msingi zipatazo 950. Idadi hii ya shule ni kubwa zaidi ya idadi ya shule katika mikoa mingine Tanzania.

Shule nyingi za sekondari ziko katika mkoa huu kwa sababu zifuatazo: 1) Hali ya hewa na vivutio vya kitalii katika mkoa huu viliwavutia zaidi walowezi na wakoloni na kuweka makazi yao hapo. Hivyo wamisionari walijenga shule za kwanza wakifuatiliwa na serikali za wakoloni 2) Serikali ya Tanzania ilirithi shule zilizojengwa na wakoloni 3) Wachaga waliobahatika kupata fedha binafsi baadaye waliwekeza kwenye ujenzi wa shule binafsi kama kitega-uchumi, wakati wakazi wa mikoa mingine kadhaa walisubiri serikali iwajengee shule. 4) Ukichanganya sababu 1, 2 & 3 utagundua shule katika mkoa wa Kilimanjaro zimezidi sana idadi ya shule katika mikoa mingine yote.

Ni vema pia kusema kuwa shule hizo huvutia wanafunzi kutoka Tanzania nzima, haziwasomeshi Wachaga tu.

**Ardhi**

Ingawa ardhi ni msingi wa maendeleo kwa watu wote, kwa Wachaga, ardhi ni mali sana kwa sababu kilimo chao ni cha mazao ya kudumu kama kahawa na ndizi hukaa shambani kwa muda wa miaka mingi.

Mojawapo ya urithi wapewayo watoto ni "kihamba". Hii ni sehemu ya ardhi ambayo mtoto anategemewa atajenga na kuanzisha familia yake. Bahati mbaya watoto wa kike walikuwa hawapewi kipaumbele katika ugawanaji wa vihamba. Uhabawa ardhi huko Uchaga ulipelekea Wachaga wengi kuhamia mikoa mingine. Hivi leo utakuta Wachaga wakiishi Dodoma, Morogoro, Iringa, Mbeya n.k. wakiwa wamepanda migomba yao na kuendesha biashara za maduka ya vyakula.

Ukienda kwenye mikoa hiyo utakuta wamejenga jamii zao na vyama vyao vya kusaidiana wakati wa sherehe au matatizo. Aidha hata pombe ya mbege utaweza kuikuta kwenye makusanyiko ya Wachaga katika mikoa mbalimbali.

**Wachaga na Wapare**

Wachaga na Wapare ni kabila kuu za Kilimanjaro. Wachaga wengi wapo Hai, Moshi, Rombo na Siha. Hii ni kwa vile wachaga waliweka makazi yao katika maeneo haya. Mwanga na Same ni sehemu za wapare zaidi.

Wachaga ni kabila ya tatu Tanzania kwa ukubwa. Waliweka makazi yao kwenye mteremko wa mlima Kilimanjaro na sehemu za jirani. Wachaga wanajulikana kwa uwezo wao wa kufanya biashara. Hii ndiyo imewapeleka kote nchini na kuwapa umaarufu.

Zaidi ya hapo, kwa kuwa hali ya hewa ya Kilimanjaro imependekeza kilimo kwa vizazi. Wachaga wametumia hali ya hewa hiyo kuweka mifumo ya umwagiliaji, uwekaji mbolea na matuta kwenye juhudi zao za kilimo. Ila, kwa kuwa walikuwa moja kati ya kabila za kwanza kuwa wakristo, walipendelewa kwa kuwa na elimu na huduma za afya bora zilizokuja na wamisionari.

Kama 90% ya kabila za kitanzania, kabila ya wachaga ni mfumo dume. Ila, siku hizi wanawake wamekuja juu na kujiendeleza sana. Katika familia nyingi siku hizi, wanawake ndio wenye mchango mkubwa kwa mapato ya kifamilia.

**Haya, twende kwa Wapare**

Wapare walikuwa wazalishaji wazuri wa chuma, ambayo ilihitajika na majirani zao wachaga. Wakawa wahunzi bora katika maeneo hayo.

Pia, walijihusisha na siasa mapema kuliko kabila nyingi sana. Umoja wa Wapare uliundwa 1946 na ulikuwa moja kati ya harakati za kizalendo Tanganyika dhidi ya ukoloni wa Waingereza. Kadri ilivyokuwa, ikajiunga na Tanganyika African National Union (TANU)

Kiuchumi, chai, kahawa na mkonge zinazalishwa kwa wingi na Wapare. Kilimo cha mazao haya kimechangia maenedeleo ya eneo hili kwa kasi sana. Ukiwalinganisha na wilaya zingine, Wapare wamejiendeleza kimiundombinu ukiangalia barabara, upatikanaji wa umeme, uunganishaji wa simu na upatikanaji wa maji.

**Kilimo na chakula**

Wachaga hulima mazao ya chakula kama vile mahindi, maharagwe, viazi, ndizi, ulezi na mboga mbalimbali. Pia mazao ya biashara kama vile kahawa, nyanya na vitunguu.

**Kilimo cha Ndizi**

Ingawa Wachaga wa leo wanakula vyakula mbalimbali kama vile ugali, wali na viazi, chakula kikuu cha Wachaga ni ndizi.

Kuna ndizi za aina mbalimbali na kwa matumizi tofauti. Mfano ndizi sukari ni fupi na huachwa hadi ziive na huliwa mbivu kama tunda.

Ndizi mshale hukatwa zikiwa mbichi na kupikiwa vyakula mbalimbali pamoja na nyama ya ng'ombe, kondoo au mbuzi. Mara nyingine hupikwa na maharage, choroko, kunde au hata maziwa ya mtindi. Vyakula vya ndizi huja kwa ladha tofauti kama vile ndizi nyama, mtori, machalari, kiburu na kadhalika.

Aina nyingine ni ndizi ng'ombe ambazo huachwa ziive halafu humenywa na kutumiwa kutengenezea pombe maarufu iitwayo mbege. Mbege hutengenezwa kwa kutumia ndizi mbivu, maji, na ulezi.

Aina nyingine ni ndizi mzuzu. Hizi zikikomaa huachwa zianze kuiva kidogo halafu huchomwa na kuliwa kama kitafunwapamoja na chai au pombe. Ukipita mitaa ya Dar es Salaam utaona ndizi mzuzu zikichomwa sambamba na muhogo au kuku vumbi au kiti moto.

**Namna Ya Kupika Machalari**

Machalari ni chakula cha asili cha wamachame wengine wanakiita ndizi nyama au ndizi za kichaga. Hizi ni ndizi zilizochanganywa na nyama, nyanya, vitunguu na viungo vingine kama mwandazi anavyopenda.

Kuna njia nyingi za kutengeneza machalari lakini ninayowaelekeza ni upikaji wa kimachame.

Vinavyotakiwa: Ndizi Mshare, Nyanya (5) Vitunguu (2), Chumvi, Mafuta ya Kupikia na Maji

1) Katakata nyama na kuichemsha mpaka ilainike halafu katakata vitunguu na nyanya uchanganye na hiyo nyama iliyochemshwa.

2) Ongeza maji kwenye huo mchanganyiko lakini yasipite juu ya huo mchanganyiko ( yawe kwenye level ya nyama) na uongeze moto hili vichemke pamoja,

3) Menya ndizi mshare na uondoe vizuri maganda. Hizi zina utomvu kwa hiyo unatakiwa umenye ndani ya maji au upake mikono mafuta. Ukishazimenya pasua katikati na uzikate kimshaazari hizo ndizi.

4)Mchanganyiko wa nyama nyanya na vitunguu uliopo jikoni unatakiwa uwekwe chumvi kidogo kutokana na ladha unayoitaji. Ikichemka weka ndizi ulizokata kwenye huo mchanganyiko.

5) Funika na hakikisha kuna moto ambao wa kadiri usioongezeka na kupungua (uwe constant) kwa muda wa dakika 20.

6) Funua na uangalie kama ndizi uliyopika imelainika halafu uweke mafuta na kuongeza maji kidogo visiungulie

7) Vikichemka ongeza maji ya mwisho yakichemka epua. Kuna wengine wanapeta kuleta mchanganyiko ulio chini kuja juu. Lakini wengine wanakoroga kupata supu mzito ya ndizi, nyanya na nyama.

8) Epua tayari kwa kula.

**Kiumbo/Kiburu**

Ni chakula maarufu pia kwa wachaga. Chakula hiki hupikwa kutokana na maharage na ndizi ambapo maharage huchemshwa na kuiva kisha huchanganywa na ndizi na baada ya kuiva

hupondwa pondwa na kutengeza kitu kama uji wa mchanganyiko huo. Chakula hicho huweza pia kusongwa na kuwa kama ugali ambao huitwa kishumba.

Kiburu huweza kuliwa na mtu wa aina na rika lolote kutokana na uandaaji wake kuwa rahisi na hakihitaji kutafuna hivyo wazee wenye shidaya meno au watoto huweza pia kula.

**Wachaga na muhogo**

Inasemekana kuwa "Mchaga halisi hali muhogo - akila muhogo atakufa". Usemi huu umetokana na historia ya mababu kuwa Wachaga waliopanda mihogo Kilimanjaro enzi za kale walikufa baada ya kuila. Historia hiyo yaweza kuwa ya ukweli kwa sababu aina nyingi za mihogo zinajenga sumu ya sianidi ndani yake; watu waliozoea kutumia mihogo huwa na njia za kuondoa sumu kwa kuiloweka mihogo katika maji kwa muda. Lakini kama Wachaga wale wa zamani, hasa wa Machame, walifanya jaribio bila kujua mbinu ya kuondoa sumu, ajali iliweza kutokea. Cha kushangaza ni kwamba hukohuko Kilimanjaro, majirani na watani wa Wachaga, yaani Wapare, walikuwa wameshazoea mihogo na ilikuja kuwa moja ya chakula chao kikuu.

**Ulaji wa kiti-moto kwa Wachaga**

Pamoja na kilimo cha mazao, Wachaga hupendelea sana kufuga nguruwe. Tabia ya kula nyama ya nguruwe ijulikanayo leo kwa jina la "kiti moto" ni moja ya mambo yaliyoenezwa na Wachaga. Ulaji wa "kiti moto" haukuwapendeza baadhi ya wenyeji wa Pwani kama Dar es Salaam ambapo Wachaga walihamia, kwani wakaaji wengi wa Pwani ni Waislamu kwa hiyo nguruwe kwao ni haramu. Wakazi wa Dar es Salaam watokao makabila mengine na wasiyo Waislamu kwao kula nguruwe ilikuwa "ruksa".

**Pombe ya Mbege**

**Mbege** ni pombe ya asili ya Wachaga, wakazi wa mkoa wa Kilimanjaro. Mbege hutengenezwa na ndizi mbivu, ulezi, na maji. Mara nyingi mbege hutengenezwa na wanawake na hutumika katika sherehe na matukio mbalimbali kama vile harusi, misiba, ubarikio, kuzaliwa kwa mtoto, n.k. Mbege hutumiwa pia kama faini kwenye mahakama za jadi. Utengenezaji wa mbege hufanywa pia kama shughuli ya kibiashara. Mbege huuzwa katika vilabu vya pombe na pia majumbani.

Pombe hii hutengenezwa kwa kuchemsha ndizi mbivu kama vile ndizi songea, ndizi uganda, kibungara, kisukari (kama zinapatikana kwa sana) n.k. Ndizi hizo zikishachemshwa huachwa kwa kipindi cha kama siku tatu au zaidi ili zichache. Baada ya hapo unga wa ulezi hupikwa na kuachwa upoe. Ndizi zilizochemshwa na kuchacha huchanganywa na maji kisha kukamuliwa ili kupata juisi yake. Juisi hiyo huchanganywa na unga wa ulezi uliopikwa na tunapata (kivuo, kifue, togwa) na kuachwa usiku mzima. Kesho yake mbege huwa tayari kwa kunywewa.

Pombe hii kama haitanywewa na kumalizika siku hiyo basi ikilala tunapata kitu kinachoitwa ngera, ambayo ni chachu sana, ila ngera pia huweza kuzimuliwa na kuwa pombe ifaayo tena kwa kuchanganya na unga uliopikwa na unga kidogo usiopikwa, ila ngera ikilala tena humwagwa kwani haitafaa kunywewa tena

Watengenezaji wengi wa pombe huwa wanaweka gamba la mti wa msesewe (Rauvolfia Caffra), hasa maeneo ya kibosho, machame na rombo ili kuongeza ladha ya uchachu na kupunguza kasi ya mbege kuchacha.

Chombo maalum kiitwacho kata hutumiwa kunywea mbege, ila mara nyingi sehemu za mijini hutumia vyombo vya plastiki, vikiwa na ujazo tofauti navyo huitwa chibuku, kideko au kitochi. Katika maeneo ya vijijini mbege hunywewa kijamaa kwa kupokezana kata. Mtu mmoja anakunywa kisha anampatia mwingine anayekunywa na kumpa mwingine.

**Dola Ya Wachaga**

Wakati wazungu wanagawana bara la Afrika, walipokuja walikuta baadhi ya maeneo kuna tawala zenye nguvu, zilizokua na mfumo rasmi wa uongozi. Wao waliziita tawala za jadi (Chiefdoms).
Moja ya tawala iliyokua na nguvu katika ukanda huu wa Afrika Mashariki ni dola ya Wachaga (Chaga state). Zilikuwepo nyingine zenye nguvu kama Himaya ya Sultani wa Zanzibar, Dola ya Buganda, Nyamwezi, Ngoni, Haya, Hutu, Tutsi na Hehe,

Dola ya Wachaga imetamalaki eneo la pembezoni mwa mlima Kilimanjaro kuanzia maeneo ya Rongai hadi Siha.

Eneo hili lilikua na mtawala mkuu mmoja (aliyeitwa Mangi Mkuu). Huyu alikua kama Rais ama Mfalme wa jamii hiyo. Chini yake walikuwepo watawala wakuu wawakilishi wa majimbo. Hawa waliitwa 'Mangi Waitori'. Chini yao walikuwepo watawala wa wa maeneo madogo, hawa waliitwa Mangi kama vile Mangi Meli wa Old Moshi, Mangi Sina wa Kibosho, Mangi Salakana wa Useri.

Kwa mfano eneo kama Rombo lilikuwa na Mangi wengi. Alikuwepo Mangi wa Keni, Mangi wa Mashati, Mangi wa Mengwe nk. Lakini wote waliunganishwa na Mangi Mwitori wa Rombo.

Vivyo hivyo katika maeneo ya Kibosho, Machame, Siha, Old Moshi, Marangu nk.

Mangi mdogo aliripoti kwa Mangi Mwitori. Mangi Mwitori naye aliripoti kwa Mangi Mkuu aliyeunganisha Wachaga wote.

Kwa mfano kufikia mwaka 1953 Mangi Mwitori wa Vunjo alikua Petro Itosi Marealle, Mangi Mwitori wa Hai alikua Abdiel Shangali, Mangi Mwitori wa Rombo alikua James Selengia Kinabo kabla ya kustaafu mwaka 1952 na John Maruma kuchukua nafasi yake.

Mangi Mwitori alichaguliwa na wamangi wadogo. Kisha wamangi wadogo na wamangi waitori waliunda baraza kuu la uongozi (Supreme council) ambalo lilimchagua Mangi Mkuu.

January 1952 kulifanyika uchaguzi wa kumchagua Mangi Mkuu wa Wachaga. Wagombea walikua watano. Abdieli Shangali wa Machame, Jackson Kitali wa Mbokomu (Old Moshi), Petro Marealle wa Vunjo, John Maruma wa Rombo, na Thomas Marealle wa Marangu.

Baada ya kila mgombea kunadi sera zake, hatimaye kura zilipigwa na Mangi Thomas Marealle kutangazwa mshindi, akifuatiwa kwa mbali na ndugu yake Mangi Petro Itosi Marealle, aliyekuwa Mangi Mwitori wa Vunjo.

Mangi Mkuu ndiye aliyekuwa Kiongozi mkuu wa dola ya Wachaga. Baraza la uongozi (Supreme council) ndicho kilikua chombo cha juu kinachosimamia utendaji wa serikali. Kwahiyo Mangi mkuu alijitahidi sana kushirikiana mangi waitori na mangi wadogo kuhakikisha jamii nzima ya Wachaga inajiletea maendeleo.

Kila Mangi alikua na baraza lake la ushauri lililojulikana kama 'baraza la wachili', ambalo lilifanya kazi kama baraza la mawaziri kwa sasa.

Ushirikiano huu ulifanya dola ya Wachaga kupiga hatua kubwa kimaendeleo kuliko jamii nyingi za wakati huo.

Kwa mfano kufikia mwaka 1920 dola ya Wachaga ilikua ya kwanza kwenye ukanda wa Afrika Mashariki kuanzisha na kumiliki gazeti lake (Komkya). Miaka 10 baadae dola ya Buganda (Buganda Kingdom) nayo ilianzisha gazeti lake (Burууli) na mwaka 1940 Himaya ya Sultani wa Zanzibar (Zanzibar Sultanate) nayo ikaanzisha jarida lake (Imperial).

Si hivyo tu, huduma za maji, umeme, miundombinu ya barabara, hospitali na shule vilifika mapema kulinganisha na maeneo mengine ya nchi. Ikulu ya kisasa ya Mangi Mkuu wa Wachaga, iliyojengwa karibu miaka 100 iliyopita ndiyo inayotumika hadi sasa kama Ikulu ndogo ya Rais kwa mkoa wa Kilimanjaro.

Zilizokuwa ofisi za watendaji wa serikali ya Mangi mkuu (eneo la KDC Moshi) ndio ofisi za Halmashauri ya wilaya ya Moshi kwa sasa.

Maendeleo haya na mengine mengi, Wachaga waliamini yalitokana na elimu. Kwahiyo mwamko wa elimu ulikua mkubwa hasa baada ya wamisionari kujenga shule na huduma za afya kila walipojenga kanisa. Vitu hivi vitatu viliambatana. Kanisa, Shule, na Kituo cha afya.

Kwahiyo hata kwenye kuchagua viongozi, yule aliyekuwa na elimu nzuri ndiye aliyepewa nafasi kubwa ya kushinda ikiaminika kwamba elimu yake itachochea kasi ya maendeleo. Na hii ni moja ya sababu iliyomfanya Thomas Marealle kushinda kiti cha umangi mkuu mwaka 1952, kwani kati ya wagombea wote yeye ndiye aliyekua na shahada ya uzamili (masters degree) kwa wakati huo.
Kabla ya uhuru kulikua wachumi wawili tu wazawa ambao ni Thomas Marealle na mzee Fredrick Mchauru ambaye walisoma pamoja London School of Economics, kabla ya Marealle kupata ufadhili Cambridge University (Trinity College).

Iliaminika pia kwamba Uingereza ilitaka dola ya Wachaga ijitenge kutoka Tanganyika na itafute uhuru wake yenyewe, kama Rwanda na Burundi zilivyojitenga kutoka Tanganyika baada ya vita vya kwanza vya dunia, wakati huo zikiitwa Ruanda-Urundi.

Hata hivyo mpango huo ulishindikana kwa kuwa Tanganyika ilikua 'Trusteeship colony' ya Umoja wa mataifa, na Uingereza alikabidhiwa tu aisimamie hadi iweze kujitawala. Kwahiyo hoja ya Muingereza ilitupwa kwa maelezo kwamba wakati wa kugawanya bara la Afrika pale Berlin mwaka 1984/85 hakuna nchi inayoitwa 'Chaga state' iliyogawanywa. Hivyo uhuru unaopaswa kuwa wa Tanganyika kwa ujumla na sio wa jamii moja moja.

Baada ya jaribio hilo kushindwa, inadaiwa shirika la ujasusi la Uingereza (M16) lilimpendekeza Mangi Thomas Mareale kuwa Rais wa kwanza wa Tanganyika baada ya uhuru.

Katika moja ya barua za Richard Turnbull (Gavana wa mwisho wa Uingereza) kwenda kwa shirika la ujasusi la nchi hiyo (M16) ilieleza mapendekezo hayo kwa Thomas Mareale.

Sehemu ya nyaraka hiyo iliyoandikwa mwaka 1958 ilisema 'I consider Thomas Marreale an outstanding Chaga leader. I dont know him personally but he would be the leader of Tanganyika if British had to leave. However he lack support from other tribes'.

Turnbull alikua akiwaelezea M16 kuhusu Mangi Thomas Marealle na umahiri wake katika uongozi. Hata hivyo alionesha hofu kuwa Marealle hakuwa na ushawishi mkubwa kwa makabila mengine nje ya Wachaga.

Na hii ni moja ya hofu kubwa aliyokua nayo Mwalimu Nyerere wakati wa kudai uhuru. Alipofika uchagani alikuta dola ya Wachaga ina mamlaka kamili. Ilikua na 'well defined leadership structure', bendera yake, wimbo wake, na askari wake.

Nyerere alisema ili Tanganyika iwe uhuru lazima dola ya Wachaga ife kwanza, kwa sababu hatuwezi kuwa na taifa moja ndani ya taifa jingine. Mwaka 1961 Nyerere aliagiza bendera ya Tanganyika isipandishwe kabla bendera ya Wachaga haijashushwa kwanza. Tarehe 8 December 1961 saa 5 usiku bendera ya Wachaga ilishushwa katika Ikulu ndogo ya Moshi, na muda mfupi baadae (saa 6 usiku, December 9) bendera ya Tanganyika ikapandishwa.

Hata hivyo hofu ya Nyerere haikua na mashiko kwa sababu Mareale mwenyewe alimpa ushirikiano mkubwa wakati wa kudai Uhuru. Na ili kuonesha kwamba hakuwa na mpango wowote wa kumhujumu, aliamua kujiuzulu nafasi yake ya umangi mkuu mwaka 1960, na kuruhusu askari wake kujiunga na jeshi la Tanganyika.

Pichani ni wagombea watatu kati ya watano walioshiriki uchaguzi wa Mangi Mkuu mwaka 1952. Kutoka kushoto ni Mangi Thomas Mareale aliyeshinda uchaguzi huo), Mangi John Maruma (Mangi Mwitori wa Rombo), na Abdieli Shangali (Mangi Mwitori wa Machame).

**Wanawake wa Kichaga**

Ingawa wanaume wa Kichaga hupendelea kufanya kazi mbali na kwao, wake zao hukaa nyumbani (Moshi) na hufuga ng'ombe na kazi za shambani. ila kwa sasa kutokana na ugonjwa wa ukimwi tabia hii imepungua miongoni mwao.

Wanawake wa Kichaga (hasa kutoka Machame) hujulikana kama wafanyakazi hodari. Huchangia sana katika mapato ya nyumbani na chakula.

Ingawa kipato cha Wachaga ni kikubwa kulingana na cha makabila mengine, takwimu zinaonyesha watoto wa mkoa wa Kilimanjaro kuongoza kwa utapiamlo. Sababu kubwa ya watoto kuwa na utapiamlo ni wazazi kujali zaidi kazi kuliko muda wa kuwahudumia watoto.

Wengi wa watoto hao ni wale ambao wazazi wao ni watu wa pombe na kipato chao kinaishia kilabuni. Utaona kwamba Uchaga una vilabu vingi vya pombe na vinaongezeka kwa sababu imekuwa biashara kubwa. Karibu kila kaya kumi na tano kuna kilabu cha pombe na kiwango cha chini kabisa cha pombe inayouzwa kwa siku katika vilabu hivyo si chini ya madebesita au lita mia moja. Pombe ni sababu moja ya watoto kuwa na utapiamlo.

Hii inawezekana kuwa matunda ya wazazi kutowalisha watoto wao chakula cha kutosha au chakula bora. Kuna sehemu nyingine za Uchaga kama Old Moshi na Kibosho ambapo watoto wadogo hupewa pombe ya mbege asubuhi, mchana na jioni.

Sababu nyingine ni kazi; mama wa Kichaga anaweza kushinda shambani kutwa na hana desturi ya kubeba watoto mgongoni kwenda nao shambani, hivyo wanakuwa nyumbani ama wenyewe

au na mayaya. Mfano ulio dhahiri ni nyakati za asubuhi na mapema kwenye vyombo vya usafiri karibu robo tatu ya abiria ni wanawake wakienda katika shuguli za biashara na kilimo na vivyo hivyo nyakati za jioni wakirudi majumbani. Hao ni nje ya wale wanaotumia usafiri wa miguu ambao ni wengi zaidi.

Pia baadhi ya kina mama wa Kichaga wanawajali waume zao zaidi kwani nyama nzuri ni ya baba. Kuepuka gharama baba ataandaliwa chakula kizuri, tofauti na chakula walichoandaliwa watoto, japo ni chakula kilekile.

Pia Wachaga wamekuwa na desturi ya kuwaenzi wazee wao waliotangulia mbele za haki kwa kuwatambikia kwa pombe na nyama za mbuzi pale tu wanaporudi nyumbani ifikapo mwezi Desemba. Hili limekuwa suala la kawaida sana na halipingiki. Wengi wao huwa wanarudi na magari, ndiyo sababu utaona ya kwambwa kila ifikapo mwezi Desemba kila mwaka foleni za magari zimekuwa zikiongezeka kutokana na Wachaga kurudi nyumbani msimu wa sikukuu. Wengi wao wamekuwa wakitoka sehemu mbalimbali za nchi na hata nje ya nchi.

Wachaga wengi hupenda kurudi nyumbani kipindi cha Krismasi, ikiwa ni kuwatembelea wazazi wao, rafiki, au ndugu.

**Dini kwa Wachaga**

Ingawa wengi hudhani kwamba Wachaga wamepokea sana dini [imani] ya Ukristo kwa kuwa wengi wao ni Wakristo na hiki huwa ni kipindi cha likizo kwao, inaaminika pia kuwa kurudi kwao Uchagani wakati wa Krismasi ni pamoja na kutembelea ndugu zao na kujumuika pamoja katika kuumaliza mwaka baada ya kazi nyingi za kutafuta pesa mwaka mzima.

Pia imekuwa kama desturi wanaukoo kukaa pamoja na kujadiliana mambo jinsi yalivyokwenda katika kipindi kizima cha mwaka na wakati mwingine inakuwa sehemu ya kwenda kuwatambulisha watoto kwa bibi na babu zao, hasa wale waliozaliwa mijini.

**Uzito na umaarufu wa jani la sale kwa Wachaga**

Sale ni moja ya majani yanayoheshimika katika mila za Wachaga kwani hutumika kwa matumizi mbalimbali. Sale hutumika kuwapatanisha watu walio katika mgogoro na endapo mmoja atakosea na kuomba msamaha kwa kutumia jani hilo hakuna sababu ya kutoukubali msamaha huo. Jani hilo limekuwa likiheshimiwa na wazee na linatumika katika mila za Wachaga tangu enzi za mababu. Jani hilo pia linatumika kuwakaribisha wageni nyumbani. Viongozi wa dini na Serikali wanapokwenda kutembelea maeneo mbalimbali katika ardhi ya Wachaga ni lazima wapokewe na jani la sale ikiwa ni ishara ya kuwepo kwa amani.

**Kwanini Wachaga hupenda kwenda kwao mwishoni mwa mwaka?**

Kumekuwa na dhana nyingi potofu juu ya Wachaga kwenda kwao kipindi cha mwisho wa mwaka, maarufu kama “kwenda kuhesabiwa”.

Je, ni kweli Wachaga huenda kuhesabiwa? Jibu ni Hapana.. si kweli. Wachaga hawaendi kuhesabiwa.

SWALI; Sasa kama hawaendi kuhesabiwa neno “kuhesabiwa” limetoka wapi na kwanini litumike kwao tu sio kwa Wasukuma, Wamasai, Wayao au Wamakonde?

JIBU; Neno “kuhesabiwa” limetoholewa kutoka neno la Kiebrania “אוֹכלוּסִין מִפקָד” linalomaanisha Wana wa Israel kurudi kwao kwa ajili ya kuhesabiwa.

Mara nyingi Waisrael walikua wanarudi kipindi cha mwisho wa mwaka wa Kiyahudi katika mwezi uitwao “Adar Beit” ambao kwa mujibu wa Kalenda ya Kiyahudi huo ndio mwezi wa mwisho wa mwaka. Na hukaa huko hadi mwezi wa kwanza wa mwaka ambao kwa kiyahudi huitwa “Nissan”.

Utamaduni huu ulitumika katika Israel ya zamani (Ancient Jews) japo kwa sasa haupo tena. Katika kipindi hiki Waisrael walikua wakikutana nyumbani na kupanga mipango ya maendeleo pamoja na kuhesabiwa ili kujua idadi yao kutokana na kutawanyika katika mataifa mengi duniani.

Tangu enzi za Musa miaka zaidi ya 4,000 kabla ya Kristo; Waisrael walikua na utamaduni wa kurudi kwao kuhesabiwa.

Katika kitabu cha 1Nyakati 23:2-3 Biblia inasema "Akawakusanya wakuu wote wa Israeli, pamoja na makuhani na Walawi. Nao wakahesabiwa Walawi wenye miaka thelathini na zaidi; na jumla yao kwa vichwa, mtu kwa mtu, ikapata thelathini na nane elfu."

Huu ni uthibitisho wa kuhesabiwa kwa Wana wa Israel zamani hizo. Lakini pia kitabu cha Hesabu 3:14-15 kinasema "Kisha Bwana akanena na Musa huko katika bara ya Sinai, na kumwambia, Uwahesabu wana wa Lawi kwa kuandama nyumba za baba zao na jamaa zao; kila mtu mume tangu umri wa mwezi mmoja na zaidi utawahesabu."

Maandiko yanayoeleza juu ya kuhesabiwa kwa wana wa Israel ni mengi na unaweza kuyasoma baadae katika (Kutoka 12:37, Waamuzi 20:14, 1 Samweli 11:8, Ezra 2:64).

Kwa hiyo kuhesabiwa ni agizo la Mungu na utamaduni huu wa wana wa Israel kurudi kwao kwenda kuhesabiwa ni utamaduni uliokua maagizo ya Mungu mwenyewe (Jehovah).

Sasa je ikiwa Wachaga hawaendi kuhesabiwa iweje wafananishwe na WaIsrael?

Sababu mbili hufanya Wachaga kufananishwa na utamaduni huu wa Israel wa kuhesabiwa.

SABABU YA KWANZA ni kitendo cha Wachaga kurudi kwao mwishoni mwa mwaka (December) na kukaa huko hadi mwanzoni mwa mwaka mpya (January). Ikumbukwe wana wa Israel nao huenda kwao mwishoni mwa mwaka wa Kiyahudi (Adar Beit) na kurejea mwanzoni mwa mwaka mpya (Nissan). Ufanano huu wa majira hufanya Wachaga nao waonekane kuwa wanaenda "kuhesabiwa" kama waIsrael.

SABABU YA PILI ni mtawanyiko wa jamii hizi mbili. Wana wa Israel wametawanyika katika mataifa mbalimbali duniani. Kutokana na ufinyu wa nchi yao wamejikuta wakisambaa nchi mbalimbali ambapo wanaishi na kufanya kazi huko. Wengine ni wahandisi, madaktari, majemadari wa vita n.k. Wana wa Israel wametawanyika mataifa yote ya Ulaya, America na baadhi ya nchi za Asia na Afrika. Pamoja na kutawanyika huku lakini mwisho wa mwaka hukumbuka kurudi kwao.

Kwa upande wa Wachaga nao wametawanyika sana katika mikoa mbalimbali nchini. Mtawanyiko wao unafananishwa na ule wa wana wa Israel kwa sababu mbili. Kwanza eneo lao la makazi (Kilimanjaro) ni dogo na haliwatoshi, sawa na Israel ilivyo ndogo na isivyotosha watu

wake. Pili ni “nature” ya mtawanyiko wao. Wachaga kama Waisrael wametawanyika sehemu mbalimbali za nchi na hata nje ya nchi.

Hakuna mkoa au Wilaya yeyote unaweza kwenda nchini ukamkosa Mchaga. Wametapakaa kila kona ya nchi wakifanya shughuli mbalimbali hususani biashara. Mtu mmoja aliwahi kutania kuwa “ukienda eneo la nchi hii ukakosa Mchaga ondoka haraka maana hapafai kuishi”.. Hii ina maanisha Wachaga wanaweza kuishi katika mazingira yoyote na hali yoyote.

Mtawanyiko wa Wachaga katika maeneo mbalimbali ya nchi hufananishwa na mtawanyiko wa Waisrael katika maeneo mbalimbali ya dunia, na hivyo basi kitendo cha Wachaga kurudi kwao mwishoni mwa mwaka hufananishwa na kitendo cha Waisrael kurudi kwao mwishoni mwa mwaka wa kalenda ya kiyahudi. Tofauti ni kuwa Waisrael huenda kuhesabiwa lakini Wachaga hawaendi kuhesabiwa.

**Siri ya Wachaga kutoingiza maiti usiku**

Ni kawaida kwa makabila mengi nchini kuzika miili ya wapendwa wao katika mikoa au maeneo ya asili ya ukoo au familia husika.

Ndio maana baadhi ya watu wanapofariki dunia husafirishwa na kupelekwa kuzikwa katika mikoa yao ya asili.

Moja ya makabila yenye utamaduni huo ni Wachaga kutoka katika Mkoa wa Kilimanjaro.

Wachaga wana mila nyingine zaidi kwani wanaposafirisha mwili wa marehemu kwenda kuuzika kijijni huwa hawaendi moja kwa moja nyumbani na hasa inapofika jioni au usiku, mwili hutakiwa kufika kijijini alfajiri, hivyo msafara huweka ‘kituo’ mahali kusubiri mpaka kunapokucha.

Mara nyingi kambi hiyo huwekwa katika baa au maeneo mengine ya karibu na kijiji wanachokwenda.

Hilo limekuwa likiibua maswali kwa watu wengi miongoni mwao wakiona kuwa huenda mila na desturi za kabila hilo zinakataza kuingiza maiti ndani usiku.

Hapa chini kuna mahojiano na baadhi ya wazee wa kichaga ambao wanaelezea kwa kifupi sababu hasa ya jambo hilo.

Louis Mbuya, mkazi wa Kilema mjini Moshi anasema watu kupumzika mbali kidogo na nyumbani kwa marehemu ni utaratibu tu ambao wamejiwekea.

Anasema si vizuri kuingia nyumbani usiku na mwili wa marehemu wakati watu wamelala kwa kuwa wataamka na kuanza kulia au kupiga kelele.

“Kunapotokea msiba na watu wanajua kwamba maiti inatoka mbali kuletwa nyumbani, huwa inasafirishwa na wakifika karibu na nyumbani usiku hawawezi kuipeleka mpaka kuche,”.

“Hakuna sababu za kimila katika hilo, hapa ni kwamba wanahofia kuamsha watu usiku kupokea maiti kwa sababu kawaida ni lazima watu walie na kupiga kelele, hivyo si vizuri kuamshwa usiku.”

Fanuel Silayo anasema utaratibu huo unatoa fursa kwa wanafamilia kujiandaa kuupokea mwili wa marehemu na ni kama heshima kwa mtu waliyempoteza.

Anasema, “Usiku watu wamelala, si vizuri kupeleka mwili na hili ni kama heshima za kuupokea mwili badala ya kuingia kimyakimya watu wakiwa wamelala.”

Silayo anasema: “Unapoona watu wamepumzika baa, hotelini au mahali pengine karibu na nyumbani kusubiri kupambazuke wanawaachia wanafamilia na waombolezaji wengine kujiandaa kwa heshima ya kuupokea msafara wenye mwili wa marehemu.”

Naye Stewart Lyatuu anaeleza kuwa, “Naomba muelewe kuwa si suala la mila, ni utaratibu na hili ni kwa sababu ya watu kupumzika na kupata chochote kwa kuwa kama mnavyofahamu maiti ikiingia nyumbani kunaibuka kelele na watu wengine hushindwa kula kutokana na majonzi ”

Agness Mushi, mkazi wa Uru, anasema tangu alipozaliwa miaka zaidi ya 60 iliyopita amekuta utaratibu huo na amekuwa akisikia kwamba wanaosafirisha maiti huwasubiri watu nyumbani wajiandae kabla ya kuwasili.

“Ni kweli wakileta maiti lazima wasubiri mahali, lakini sijui kama kuna sababu za kimila,” anasema.

“Jambo jingine ambalo nimeliona pia ni kwamba kama kaburi limeshachimbwa halafu maiti ikachelewa kuzikwa siku hiyo, lile kaburi haliachwi, yaani wachimbaji watabaki huko kuendelea kuchimbachimba hata na kijembe kidogo hadi maiti ifike.”

Anasema wachimbaji wanaweza kukesha katika eneo la kaburi wanachimbachimba.

“(Hii hutokea) wakati mwingine watu wanaweza kuwa wanasafirisha maiti halafu ikatokea ajali wakashindwa kufika, hivyo wachimbaji huwa wanabaki kule kuonyesha kazi ya uchimbaji inaendelea mpaka maiti itakapofika nyumbani.”

Wakati hao wakisema huo ni utaratibu wa kawaida, Profesa John Boshe, mkazi wa Kibosho, anasema suala hilo linatafsiriwa kwa namna mbili wakiwapo wanaodai kuhofia taharuki na wengine imani na kuogopa mikosi.

Anasema wanaoogopa kufikisha maiti nyumbani mapema huhofia kuibua taharuki na kelele.

“Kumfikisha marehemu mapema nyumbani kunaweza kuleta taharuki kwa wafiwa na majirani kuanza kuomboleza mapema na kupiga kelele, haipendezi,” anasema Profesa Boshe.

Jambo la pili, anasema, ni imani na mila, kwamba mwili wa marehemu ukifikishwa unatakiwa kwenda kuzikwa moja kwa moja.

Anasema pia wapo wanaoamini kwamba mwili wa marehemu ukiwekwa ndani unaweza ‘kumvuta’ mtu mwingine akafa, na imani hiyo iko kwa baadhi ya watu na si Wachaga wote.

“Hii ndiyo maana kaburi huandaliwa siku hiyo mapema na maiti ikifikishwa nyumbani huingizwa kwenye nyumba anayotakiwa kuingizwa na akitolewa anapelekwa kaburini.”

Hata hivyo, Silvester Temba anasema hakuna sababu za kuendelea na imani hiyo kwa vile haina madhara kwa wafiwa au watu wengine.

“Sioni sababu ya kuendelea kuamini mila zilizopitwa na wakati kwa kuwa toka tumezaliwa tunaona hayo yanatendeka, lakini hatujawahi kushuhudia madhara kwa watu ambao wamekuwa hawaamini mila hizo”.

**Kufufu wafu**

**Edward Lyimo, akionyesha fuvu  la baba yake mzazi**

Ni jambo linaloweza kuwa geni kidogo kwa baadhi ya makabila, lakini kwa baadhi ya Wachaga wa Kilema mkoani Kilimanjaro kuna mila ambazo kwa makabila na jamii nyingine zinaweza kuwa za kushangaza.

Jamii hii inaonekana kuwa tofauti na Wachaga wengine kwani wao huwafukua wapendwa wao waliofariki kila wanapotimiza miaka minane hadi 10 baada ya kuzikwa.

Mila hiyo ina taratibu zake za kufuata kabla ya kufikia hatua ya mwili kufukuliwa sehemu ulikokuwa umezikwa na kwenda kuhifadhiwa sehemu nyingine.

Kitendo cha kufukua maiti kimekuwa kikifanywa kwa kufuata taratibu maalumu za kimila na zisipofuatwa inaaminika huwa na madhara makubwa kwa ukoo ikiwamo kusababisha kifo.

**Wenyewe wanasemaje?**

Mmoja wa wanaukoo wa Lyimo, Edward Lyimo anasema utamaduni huo aliukuta tangu akiwa mdogo na unaendelea mpaka sasa akiwa mtu mzima.

“Si jambo la ajabu. Katika utu uzima wangu nimeshafukua ndugu zangu wengi tu waliokufa miaka ya nyuma na kuihifadhi eneo maalumu lililotengwa na familia kwa ajili hiyo,” anasema.

Anasema sherehe hufanyika kimila kwa kutumia jani maalumu linaloitwa sale kwa kuchomekwa kwenye kaburi la marehemu ambapo hufukuliwa siku moja baada ya kuwekwa kwa jani hilo.

“Kuna mzee maalumu ambaye anasimamia hatua zinazotakiwa kufuatwa na ndiye anafanya zoezi hilo la kuwafukua marehemu ambao miaka yao imekwishafika,” anasema na kuongeza kuwa mzee huyo ndiye mtu pekee anayefanya kazi hiyo.

Lyimo anafafanua kuwa inatakiwa kila ukoo unaofanya mila hiyo uwe unajua taratibu za kufukua, lakini kutokana na ugumu wa mila hiyo imekuwa ikishindikana kwa baadhi ya watu.

“Kulikuwa na wazee wawili ambao walikuwa wanafanya kazi hiyo na tulikuwa tukiwaona lakini wameshakufa na kulikuwa na mzee maarufu sana kwa mila na kuvunja laana,” anaeleza.

Anasema mzee huyo ndiye aliyekuwa akifanya mila hizo kijijini kwao na alikuwa na uwezo wa kuzunguka sehemu nyingi kusaidia watu katika mila zao.

Lyimo anasema baada ya mzee huyo kufariki, sasa wanamtumia mtu mwingine aliyerithi utaalamu huo wa kufukua maiti.

**Mila ya kufukua maiti**

Anaelezea kuwa ndugu wao anapofariki na kutimiza miaka minane baada ya kufa, huwa anaanza kuwatesa familia kama hawatamfukua kama mila zao zinavyoelekeza.

“Asipofukuliwa kunakuwa na mikosi, hivyo lazima tufanye hilo tambiko na kwa kuwa familia haina utaalamu huo, inabidi tuandae vitu vyote vinavyohitajika na kisha tunamuomba mtu wa mila atusaidie”.

Siku moja kabla muda wa saa 10:00 alasiri, yeye (mzee wa mila) anaotesha jani la sale pamoja na kumwaga pombe ya mbege kwenye kaburi ambalo mtu anatakiwa kufufuliwa. Kesho yake mzee huyo huenda kaburini kuliangalia jani hilo kama limenyauka au la. Kama halijanyauka ni ishara ya kwamba wakifukua kaburi hilo watakuta fuvu la mhusika.

“Nikikuta sale halijanyauka mbuzi anachinjwa na kunena maneno yanayotakiwa kuzungumzwa wakati namwaga damu ya mbuzi katika kaburi hili,” anasema na kuongeza: “Kisha wanaukoo wanaanza kufukua kaburi huku akiwaelekeza vitu vya kufanya.”

Anasema wanaukoo hufukua kaburi huku kina mama wakiendelea na shamrashamra za kupika maana inakuwa ni sherehe kubwa.

Anasema mara tu wanapoanza kuona mabaki ya marehemu wanasitisha kila kitu, huku wanawake wakiruhusiwa kusogelea eneo hilo na kuanza kupiga vigelegele.

Anasema kina mama wakishapiga vigelegele wanaanza kuwapa watu chakula kilichoandaliwa na huwa wanakaa sehemu husika siku nzima kwa sababu kazi hiyo huchukua muda mrefu hivyo inawabidi kula na kunywa.

Anasema baada ya vigelegele kumalizika, fuvu la mhusika linachukuliwa na kufungwa kwenye majani ya sale na kisha kuhifadhiwa ndani.

Fuvu hilo likishahifadhiwa ndani ni ishara kuwa mtu huyo yuko hai na si mfu tena kwa mila na imani za Wachaga wa Kilema.

“Nikishaliweka ndani naendelea kutafuta mabaki mengine ndani ya lile kaburi maana ukibaki hata msumari wa jeneza, tuliokuwa tunafanya kazi ya kufukua tunapatwa na mauzauza ya kutolala.”

Anasema kesho yake huamka asubuhi mapema na kuchukua fuvu hilo na kulisafisha kwa kulipaka mafuta ya ‘msuka samli’ na kisha kulifanyia mila nyingine.

“Baada ya hapo nalishikilia na wanaukoo wanakuja mmoja mmoja kuja kulipaka fuvu hilo mafuta. Wakati wakipaka mafuta kwenye fuvu hilo, kila mtu anakuwa akiomba mahitaji yake.”

Anasema baada ya kupaka mafuta fuvu hilo huwa analibeba na kupeleka sehemu ya kulihifadhi akiandamana na baadhi ya wanaukoo kwa idadi sawa ya jinsi.

Lyimo anasema wakiwa wanaelekea sehemu hiyo aliyoiita ‘Mbuoni’ huwa hawaruhusiwi kugeuka nyuma hadi wanapofika sehemu wanapoweka fuvu hilo.

Anasema mara baada ya kuhifadhi fuvu hilo sehemu husika, hurudi na kuendelea na sherehe za kimila.

**Sababu ya mila hiyo**

Mwenyekiti wa kitongoji cha Kyuo, Aloyce Lyimo anasema sababu ya kufanyika kwa mila hiyo ni ufinyu wa ardhi hali inayosababisha wananchi kuendeleza mila hiyo ya tangu enzi za mababu.

“Miaka ya sasa watu wanakufa kwa wingi na tukisema tusiwafufue vizazi vyetu vitakosa mashamba ya kurithi kwa kuwa makaburi yatakuwa kila kona ni mila nzuri na ya kuigwa.

Anasema kuwa zamani wazee walikuwa hawaziki, bali walikuwa wanahifadhi mwili huo ndani na baada ya miaka miwili wanachukua masalia na kuyahifadhi sehemu iliyotengwa.

**Siri Ya Wachaga Kuzika Kwenye Vihamba**

Na Daniel Mjema, Mwananchi

**Moshi**. Agizo la Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi ya kutaka kutengwa maeneo ya maziko katika Mkoa Kilimanjaro imeibua mjadala huku suala la kuenzi mila likitajwa kuwa ni sababu ya kuzika kwenye vihamba.

Baadhi ya wananchi wa Kilimanjaro waliohojiwa na Mwananchi wamesema, kimila ni lazima marehemu azikwe kwao ambako kitovu chake kilizikwa, tofauti na hivyo huleta balaa kwa familia.

Wakazi wa hao Wachaga wa wilaya za Rombo, Hai, Moshi na Siha, wana utamaduni wa enzi na enzi wa kuzika ndugu zao katika mashamba madogo ya maeneo yao ya asili maarufu ‘vihamba’.

Lakini wiki iliyopita Waziri Lukuvi aliziagiza halmashauri zote za mkoa huo, kutenga maeneo ya jumuiya kwa ajili ya maziko, ili wakazi wa mji huo waone umuhimu wa kuzika kwenye makaburi hayo.

Mangi Marealle, wadau wafichua siri

Kiongozi wa Kimila ambaye ni Mangi wa Wachaga wa Marangu, Frank Marealle, alisema sababu ya wakazi wa maeneo ya uchagani kuzika kwenye vihamba ni mila na desturi za kabila hilo.

Mangi Marealle ambaye alimrithi Chifu Agustino Marealle aliyefariki dunia mwaka 2006, alisema kwa mila za Wachaga, mtoto wa kwanza na wa mwisho katika familia lazima wazikwe kwenye kihamba.

“Hizi ni mila tu kwamba kwa mfano ukiwa na watoto watatu. Yule wa kwanza na wa mwisho ndio wanagawiwa kihamba kila mmoja. Kama eneo litabaki ndio atapewa huyo wa katikati,” alisema.

Alisema watoto hao wanapokufa, huzikwa katika vihamba vyao lakini kwa sasa kuna shida kutokana na uhaba wa maeneo, na wanatafakari mustakabali wa siku za usoni.

“Tunafikiria tuachane na huu utaratibu au tuendelee kuzika,” alisema na kueleza kuwa hata agizo la Lukuvi litapata changamoto ya maeneo ya kuzikia.

Mkazi wa Machame, Basil Lema alisema mtoto anapozaliwa, kitovu chake hakitupwi ovyo, lazima kizikwe kwenye eneo la familia na ndipo pia atakapozikwa.

“Hata kama mtoto amezaliwa New York (Marekani), lazima ukitunze hicho kitovu na kukirudisha huku nyumbani na kuna mila zake, ni lazima hapo kinapozikwa paoteshwe mgomba,” alisema Lema.

Hata hivyo, Lema alisema katika siku za karibuni, waumini wa Kikristo walianza kuzika katika maeneo ya jumuiya ya kanisa ambayo nayo yamejaa na sasa baadhi wamerudi kwenye vihamba.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Shirimatunda, Beda Massawe, alisema utaratibu wa kuzika kwenye vihamba wameukuta na upo tangu enzi za mababu, na wao wamerithi kama mila na kuiendeleza.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi, Michael Mwandezi alisema ofisi yake ina maeneo matatu kwa ajili ya maziko.

“Tuna maeneo Karanga, Njoro na Pasua na hapo Bondeni karibu na TBL na tumenunua eneo lingine huko Mtakuja Moshi Vijijini.”

Alisema sheria za manispaa zinazuia mtu kuzikwa katika eneo lake lililopimwa isipokuwa kwa kibali maalumu.

Mwandezi alisema maeneo ambayo watu huzika kwenye vihamba ni yale yaliyo nje ya manispaa hiyo na ambayo hayajapimwa.

**Sikukuu ya Wachaga**

Sikukuu ya Wachaga wote ilikuwa ikiadhimishwa Novemba 10 kila mwaka kama kumbukumbu ya siku ambayo Wachaga wote walipokusanyika na kumchagua Mangi Mkuu baada ya kuteuliwa na Halmashauri Kuu ya Uchaga.

Maadhimisho ya kwanza ya mwaka 1952 yalitanguliwa na uchaguzi wa Halmashauri ya Wachaga wote kuanzia kwenye ngazi ya Uchili (kijiji), Umangi ( uchifu wa eneo) na mwisho ngazi ya baraza kuu.

Sherehe ziliadhimishwa mjini Moshi ambako Wachaga wote pamoja na wageni waalikwa kutoka mataifa mbalimbali walikusanyika katika Viwanja vya Halmashauri ya Uchaga (sasa ni makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, [Kilimanjaro District Council-KDC]) kushuhudia sherehe kubwa na yenye kusisimua sana.

**Jumba la Makumbusho**

Upo umuhimu mkubwa wa kuhifadhi historia ya Wachaga kama kumbukumbu sahihi kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Pia, ipo haja kwa majengo ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi pamoja na Ikulu yakarejeshwa kwa Wachaga ili yageuzwe kuwa majengo ya kuhifadhi kumbukumbu ya kabila hilo.

Katika majengo haya patahifadhiwa nyaraka zote za Chaga Council ambazo baadhi zimeshaanza kutoweka, kutahifadhiwa pia shughuli za mila na kiutamaduni tangu enzi ya karne ya 18.

Halmashauri ya Wilaya ya Moshi haina budi kutafuta eneo la kujenga majengo mapya badala ya kuyatumia ya kihistoria.

**Kama Wachaga hawahesabiwi, wanaenda kufanya nini?**

Pengine hili ndio swali la msingi ambalo wengi wanajiuliza. Ikiwa Wachaga hawaendi kuhesabiwa kama ilivyo kwa waisrael, Je wanaenda kufanya nini?

Ukweli ni kwamba Wachaga wanakwenda kwao kwa sababu mbalimbali. Leo nitaainisha kwa uchache sababu 10 zinazorudisha Wachaga kwao kila mwisho wa mwaka. Zipo nyingi zaidi ila kwa kifupi ni kama ifuatavyo;

1. Kuna wanaokwenda kwao kwa ajili ya kuonana na familia zao na kuwaona wapendwa wao na kujumuika nao kwa ajili ya kufurahia sikukuu za mwisho wa Mwaka huhusani “Krismasi” na “Mwaka mpya”.

Kwa mfano wazazi wako (baba na mama) au ndugu zako wengine (babu, bibi, kaka, dada, shangazi, wajomba n.k) hujawaona kwa kipindi cha mwaka mzima. Mmekuwa mkiwasiliana tu kwa simu. Hivyo basi Desemba huwa ni kipindi kizuri cha kurudi nyumbani na kuwaona na kuwajulia hali.

2. Pia kipindi hiki hutumika kupanga mipango ya maendeleo ya familia kama vile kujenga. Kwa kuwa watoto wote wa familia hukutana kipindi hiki basi huweka mipango ya maendeleo kwa

familia yao. Wanaweza kupanga kujenga nyumba kwa ajili ya wazazi wao ambao ni wazee, kuweka umeme, maji n.k.

Uchagani ni mojawapo ya maeneo nchini ambako kuna nyumba nyingi za kisasa vijijini na ni mkoa uliofanikiwa kupiga vita nyumba ya Nyasi tangu mwaka 1996.

Ni jambo la Kawaida kukutana na maghorofa ya kisasa kule "Machame Uswaa, Kibosho Kirima, au Mamba Komakundi".. au ukipita "Uru Mawela, Rombo Mamsera au Kilema Poffo" nyumba zote unazokutana nazo ni 'self-contained' za kisasa, lakini wanaishi wazee. Watoto wao wapo Shinyanga, Dar, Kigoma, Mwanza n.k wanatafuta maisha. Mipango hiyo ya kujenga na kuhudumia wazazi hupangwa msimu huu wa sikukuu za mwisho wa mwaka.

3. Msimu huu wa sikukuu hutumika kupatanisha ndugu, jamaa au marafiki waliokosana. Wazee huitwa na kuzungumza na pande zote mbili kisha kuwapatanisha. Mkikubali kuelewana basi huchinjwa mbuzi kama ishara ya furaha ambapo jamii yote hujumuika kwa kula na kunywa.

4. Kipindi hiki cha msimu wa sikukuu ndio kipindi kizuri ambacho vijana hukitumia kutambulisha wachumba zao nyumbani. Unaweza kuwa unaishi Dar na umepata mchumba wa Morogoro. Lakini ndugu zako wametawanyika. Wengine wapo Tabora, wengine Mwanza, wengine Mbeya. Huwezi kupita na mchumba wako kote huko kumtambulisha. Kwahiyo "option" nzuri ni kusubiri msimu wa sikukuu za mwisho wa mwaka ambapo ndugu zako wote watakuwepo nyumbani ndipo umpeleke mchumba wako kumtambulisha, na kupanga mipango ya ndoa.

5. Kuwaleta watoto wafahamu ndugu zao na wafahamike nyumbani. Unaweza kuwa unaishi Dar na familia lakini ndugu zako wanaishi na familia zao maeneo mengine ya nchi, watoto wenu hawafahamiani maana hawajawahi kuonana. Hivyo mkikutana nyumbani msimu wa sikukuu ni kipindi kizuri cha watoto wenu kufahamiana na kufahamu asili yao.

Pia ikiwa umejaliwa mtoto ukiwa huko unakofanyia shughuli zako lakini wazazi wako hawajamuona mjukuu wao, hiki ni kipindi kizuri cha kuwapelekea wazazi wako mjukuu wao wamuone na kumpa baraka.

6. Kushiriki shughuli za kijamii (charity work). Wachaga wengi ni waumini wazuri sana wa dini iwe ukristo au uislamu. Hivyo kipindi cha msimu wa sikukuu hutenga muda wa kutembelea wagonjwa, Yatima na Wasiojiweza na kuwapa misaada mbalimbali. Kwa wale Wakristo huita "Sadaka ya Epifania".

7. Kipindi hiki hutumika pia kufanya usafi na kurekebisha maeneo waliyopumzika wapendwa wetu (makaburi). Wachaga kama ilivyo binadamu wengine hutenga maeneo maalumu ya kuzikia ndugu zao; na mara nyingi kila familia ina eneo lake.

Kwa hiyo ikiwa kuna ndugu amefariki na akazikwa basi msimu huu huwa ni kipindi kizuri cha kujengea makaburi kama kumbukumbu ya sehemu walipopumzika wenzetu.

Bahati mbaya wapo watu wanaohusisha utamaduni huu na matambiko. Kwanza ieleweke kujengea makaburi si dhambi na si matambiko. Hata Yakobo alipofia kule Misri alipoenda kwa mwanae Yusufu alizikwa kwenye Kaburi lililojengewa (Matendo 7:15-16). Hivyo basi ni vizuri ikaeleweka kuwa kujengea makaburi si dhambi.

Na mara nyingi uchagani kabla ya kujengea Kaburi kiongozi wa dini huitwa na kufanya sala, kabla ya shughuli ya ujenzi haijaanza. Kwahiyo hakuna nafasi ya matambiko.

Ikiwa kuna mchaga anafanya matambiko wakati wa kujengea makaburi ichukuliwe kuwa ni tabia ya mtu binafsi na isihuhishwe Wachaga wote. Kwani wapo watu wa makabila mengine hufanya matambiko pia lakini huwezi kusema jamii yote hutambika.

8. Msimu huu wa sikukuu ni kipindi kizuri ambacho Wachaga hukitumia kupanga na kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo ya jamii yao kama vile mashule, hospitali, Maji, barabara n.k

Kwa mfano zipo barabara nyingi ambazo zimejengwa kwa nguvu ya wananchi wenyewe kwa kuamua kujichangisha bila kusubiri serikali ifanye. Barabara ya Uru Kusini ni mojawapo. Mipango hii hupangwa msimu huu wa sikukuu.

9. Msimu huu hutumika kwa ajili ya mapumziko ya familia baada ya mahangaiko ya mwaka mzima. Ni wakati wa familia kutulia pamoja kutafakari mipango ya mwaka uliopita na kuweka mipango mipya ya mwaka unaofuata.

Ndugu na jamaa hukutana pamoja na kufurahia sikukuu za “Krismasi” na “mwaka mpya” kwa kula na kunywa hasa vyakula vya asili kama “kisusio, faya, supu ya mbuzi iliyopikwa kiasili kwa kuchanganywa na majani aina ya “mahombo” na vyakula vingine bila kusahau kinywaji aina ya mbege.

10. Kipindi hiki hutumiwa kujenga na kukarabati nyumba za ibada. Ni wazi kuwa Kilimanjaro ni miongoni mwa maeneo ambayo kuna nyumba nzuri na za kisasa za Ibada.

Kanisa kubwa na la kisasa kama la KKKT Old-Moshi Rau, au La RC Kristu Mfalme, Au TAG Kilimanjaro Revival, au Msikiti wa kisasa kama wa Riadha, ni nadra kuvipata mahali pengine. Au Kanisa la kale kama la KKKT Old-Moshi Kidia lililojengwa mwaka 1843 utalipata wapi kwingine?

Mipango ya ujenzi wa nyumba hizi za ibada za kisasa na kukarabati zile za zamani hufanywa msimu huu wa sikukuu.

Pia Wachaga wengi hupenda kwenda kwao kwa kuwa ibada zote katika msimu huu huongozwa kwa kichaga. Yani kuanzia usomaji wa misa, mahubiri hadi nyimbo huimbwa kwa kichaga, wakati huo nyumba za ibada zimepambwa kwa mapambo ya asili kama “Makurera, makangachi, migomba imechimbiwa vichumini (njia za kwenda nyumbani)” n.k.

Hii huongeza nakshi na kufanya mtu ajisikie kupungukiwa kitu ikiwa hatakuwepo Nyumbani msimu huu wa sikukuu za mwisho wa mwaka.

Utamaduni huu wa Wachaga ni mzuri sana, na kuna mengi jamii nyingine zinaweza kujifunza kupitia Wachaga kama ambavyo Wachaga wanaweza kujifunza kupitia jamii nyingine.

**Nyumba za asili za Wachaga**

Wachaga kabla ya kupiga hatua za kimaendeleo kufikia hivi walivyo sasa walikuwa wakijenga na kuishi katika nyumba za asili za msonge kama ilivyo kwa makabila mengi nchini Tanzania. Nyumba hizi kuzungukwa na minanasi ambayo kwa asili ina miiba ili kuzuia nyoka wasiweze kuingia ndani ya nyumba na kuleta madhara.

**Bendera Ya Wachaga**

Halmashauri ya Uchaga ilikuwa na bendera yake ambayo ipo hadi leo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, yenye nembo tano kuu:

1- Mlima Kilimanjaro uliochorwa katikati ya bendera ukionyesha mandhari nzuri ya kilele cha Kibo. Kilele cha Kibo kinatoa maji safi na ni kielelezo cha umoja wao.

2- Chini ya kilele cha Kibo, upande wa kushoto wa bendera kuna mgomba wenye ndizi. Hiki ni chakula kikuu cha Wachaga.

3- Upande wa kulia wa bendera ni tawi la mbuni ukiwa na matunda yake. Kahawa ni zao lililowaletea maendeleo.

4- Bendera imezungukwa na matawi ya 'sale' lenye matawi mawili (draceana plant). Matawi haya yamefanya mduara kuzunguka kilele cha Kibo, mgomba wa ndizi na tawi la zao la kahawa. Masale ni mmea unaoheshimiwa sana na Wachaga wote.

Ni alama ya amani. Masale hutumika katika sherehe na shughuli zote za kimila zinazofanywa na Wachaga. Majani yake ni kijani kibichi yanayoonyesha jinsi Kilimanjaro ilivyo na rutuba nzuri inayostawisha mazao ya kila aina.

5- Juu kidogo ya kilele cha Kibo yupo chui ambaye amejipumzisha. Chui ni alama kuu ya mamlaka ya Wachaga.

Hapo awali kwenye miteremko ya Mlima Kilimanjaro walikuwepo chui wengi wa rangi nyeusi lakini kutokana na ongezeko la watu pamoja na uharibifu wa mazingira chui hawa wametoweka.

**Baadhi ya maneno ya kichaga**

**NENO NA MAANA YAKE**

**S**himboni -- Shikamoo --(Habari yako?)

**S**himboni mae/mbe -- Shikamoo mama/baba?

**N**asicha -- Nzuri

**A**ika --Ahsante

*mae/mbe yanaweza kuwekwa mbele ya neno lolote la salamu m.f.) "Aika mae" "Aika mbe" **A**ika mana -- Ahsante mtoto

Rakucha,**l**akucha-- Usiku mwema

**C**hamecha Pole na...(hasa kwa safari)

**O**tana -- Pole na kazi.

**O**kora mae -Ahsante mama kwa kunipikia chakula

(Okora mae lipo ila huwezi kusema "Okora mbe" useme tu "Aika mbe" kama baba akipika chakula labda)

**N**okyelaonacho? **N**ukelaho u? - Unaitwa nani?(hii inategemea ni mchaga wawapi)

**N**gikyelao? **N**jikelaho? ~~~ Naitwa ~~~

**O**roka, **H**oroka-- Simama

**R**amia, **D**amia-- Kaa

**T**ikira --Sogea **S**hinde! **N**nde-- Twende!

**N**gicho njaa mae , **N**jiicho Njaa mae-- Nina njaa mama

**N**gacho gicho kie , njiicho njichokie -- Nimechoka

Gayuja mae, Ngaihuda mae- Nimeshiba mama

Ngicho nbeyo,njiicho mbeo-- Nina baridi

Ngicho mrike,njiicho mrike Ninasikia joto

maruwa-- maziwa

(Ruwa ina maana ya Mungu kwao katika kichaga ila hapa "maruwa" halihusiani na Ruwa)

memba--Ndizi

Maimba --mahindi

mbuya –rafiki

Aichi—Anajua

iachikyia--Kujenga

Ichele—Kichaga

Ichondi- --- Kondoo

Iikyelyia—Kuogelea

Ikawilyia—Kupalilia

Ilyingoi---Jogoo

inyi—Mimi

Ipalipali- --Bahari

Ipore---Yai

Irikoso—Taji

Isewa—Kibuyu

Itukuo—Kushangaa

Iwuwu—Kuona makengeza

Iyesho---- Majaribu

Kiamba---Shamba

Kyasaka—Ugenini (Mswahili)

Kyiaatyi—nafasi

Kyo_kyimaryu—Ndiyo sababu

Kyuwere—Kumebakia nafasi ndugu

Lakucha—Usiku mwema

Linyala—Kuzarau

Maakulembecherye—Unafiki

Mapore—Makande

Mapuchi—Mawingu

Masaanga—Mataifa

Matu matu—Tafadhali

Mbuya---Rafiki

Mchola--Kichochoro

Mkuuchu—Kiburi

Mkuuma---Upepo

Mlenya—Mchanga

mmesa—Adui Mtiima—Giza nono

Mmmbaryi—Jua

Momrasa—Jirani

Momu- hori la ng’ombe

Msasariko—Masazo

Msotsa---Kushuka

Na-Ngoseraa—Na zaidi

Ndekye—Ndege

Nduwa-- Dimbwi

Ngambura--kipande cha nyama

Njoonyi—Ngozi

Nyi Kryirumi—Ni Utukufu

ote=hapana

Parapara—barabara

Pfinya—Nguvu

Rumbu—Mdomo

Sera'—Mgomba mchanga

Shira'—vita

Tao—Ng'ombe jike

Tikira- sogea

ukou=Jana

Ulakuso—Tafadhali

Ulowo—Habari

Unga—msoo

Unyamari'—Dhambi

Ushanguny—Usoni

Walutsa—Geuza

Wanda—chini

**Utani wa Wachaga**

**Wachaga wamegawanyika kama ifuatavyo, sio wote wajanja. Kuna:-**

1. WAROMBO; Hawa wajanja sana kibiashara/wezi pia. wanapenda dili za magendo. Ni walevi sana hupeleka wake zao vijijini wakileta kiburi mjini. Wanaume wa Rombo wanachunwa sana na wanawake wa Marangu na wanawaita "vishohia". Wanawake wa Rombo ni mama Huruma, wanaachia tu.. Ukioa Mrombo ujue umeolea kijiji.

2. WAMARANGU; Ni wazuri sana wa sura na umbo, wanavutia. Lakini wanawachuna sana Warombo. Wanawake wa Marangu wana dharau sana na wanaume ni waoga kuliko wanawake. Mwanaume wa Marangu kupigwa na mkewe si jambo la ajabu.

3. WAKIBOSHO; wanafanana na Warombo lakini ni wavumilivu zaidi. Biashara kubwa wanayofanya ni ya kuchinja... wengi wanamiliki mabucha. Wana hasira sana na ni wakatili.. Akikuchoma kisu, siku ya mazishi anakuja kudai kisu chake.

4. WAMACHAME; hawa ni wezi sana, ukifanya nae dili umeliwa. Ni wasiri sana lakini wako makini mno hasa kwenye pesa. Wakiwa na hasira hawaoneshi waziwazi, so Mmachame anaweza kukuua huku akitabasamu. Sio waaminifu sana lakini wanaenda kanisani mara nyingi zaidi kuliko Wachaga wote. Wanawake wa machame wanaitwa 'Wapalestina'.. Mume ukitajirika mkeo anakuua ili arithi mali.

5. WAURU; hawa hupenda kusoma sana lakini hawapendi maendeleo kabisa. Hadi leo eneo lao la Kishumundu linatumika ku-identify wachagga washamba. Wanawake wakifikisha umri wa miaka 40 hua wehu na wanaume huwa vichaa mapema zaidi. Wanaume ni wavivu, lakini wanawake ni wachapakazi hodari. Wanazurura mjini na mabeseni wakiuza ndizi mbivu.. Ukioa Uru jiandae kulea kichaa.

6. WASIHA; Kwanza hawapendi kuitwa Wachagga. Wanajiita watu wa West-Kilimanjaro. Ni mchanganyiko wa Wachagga na WaMeru. Hawapendi shule ila wanapenda zaidi kazi za ufundi na kilimo. Viazi vingi vya Chips Arusha na Moshi vinatoka kwao. Wanawake zao wana "vigimbi" mguuni sababu ya kulima mno.!

7. WAKIRUA; wanapenda sifa kama Wahaya. Wanawake wa Kirua ni wachawi kupindukia..

Wanaloga hata jiwe ili tu alikomoe.. Wanaume wa Kirua hawapendi kuoa kwao.. Hawapendi kuishi mjini maana wanaogopa gharama.. lakini siku wakija mjini wawili tu utadhani wako mia.

8. WA OLD-MOSHI; Hawa ni mafundi stadi wa ujenzi wa nyumba, japo hawajengi kwao. Mpaka leo hamna daladala ya kwenda Old-Moshi inayoanzia Moshi mjini, maana ni wabishi kulipa nauli na pesa inaishia kwenye mbege njiani. Wanaume wamezoea kutoka nyumbani saa kumi na moja alfajiri na kurudi saa sita ya usiku kwa miguu.!

**Umaarufu wa Ndafu kwa Wachaga**

Ndafu ni aina maalumu na maarufu ya uchomaji wa mbuzi aliyehasiwa na kutunzwa vizuri ambaye huokwa na kupambwa ili kutumiwa kama keki ya heshima kwenye sherehe hususani harusi. Inadaiwa kuwa neno NDAFU lilitokana na mzungu mmoja aliyetembelea uchagani na kukuta aina hiyo ya kitoweo alipoonja akaishia kusema “Wonderful” neno ambalo wachaga walishindwa kulitamka na kuishia kutamka NDAFU na tangu hapo neno hilo likaenea na kutumiwa rasmi kwa aina hiyo ya uchomaji wa mbuzi.